## *Kadi ya Miadi*

Kwa ajili ya: ________________________________

Tarehe: ______________ Muda: ______________

Mfanyakazi wa PghCHR:

________________________________________

## *Jinsi ya kuwasiliana na PghCHR*

Anwani: 908 City-County Building (Ross St. Side)
414 Grant Street
Pittsburgh, PA 15219

Simu ya Ofisini: (412) 255-2600

Tovuti: www.pittsburghpa.gov/chr

Barua Pepe: human.relations@pittsburghpa.gov

Tufuatilie kwenye mitandao ya kijamii @PghCHR

*Taarifa za sasa hadi kufikia Juni 2023.*

# *Zijue Haki Zako*

*TUME YA UHUSIANO WA BINADAMU YA PITTSBURGH (PghCHR)*

[Swahili]

*Tunatoa Haki kwa Kushirikiana*

**Tume ya Pittsburgh ya Mahusiano ya Binadamu (Pittsburgh Commission on Human Relations)**

## *Kuhusu PghCHR*

- Tume ya Uhusiano wa Binadamu (PghCHR) huchunguza matukio ya ubaguzi katika makazi, ajira, malazi ya umma na katika utoaji wa huduma, ikiwa ni pamoja na polisi.
- PghCHR inatafuta maridhiano kwa mtu yeyote aliyeadhiriwa kwa sababu ya ubaguzi.
- Sisi ni zaidi ya shirika tu linalotekeleza sheria. Tunafanya kazi na jumuiya na mashirika ya umma na binafsi, ili kuwaelimisha watu mapema kuhusu haki na fursa sawa.

## *Ubaguzi ni Nini?*

- Ubaguzi humaanisha tofauti katika ushughulikiaji kwa sababu ya kuwa mtu wa **tabaka linalolindwa**.
- Tabaka linalolindwa ni kikundi cha watu wenye nasaba sawa ambao wanalindwa kisheria wasibaguliwe kwa sababu ya nasaba yao.
- Katika jiji la Pittsburgh, matabaka yafuatayo yanalindwa:
    - **Ajira:** Umri, Ukoo, Rangi, Ulemavu,Utambulisho wa Jinsia, Ubainishaji wa Jinsia, Vitambaavya Nywele na Kichwani, Asili ya Kitaifa,Ujauzito, Mahali pa Kuzaliwa, Mbari, Dini,Jinsi, Mwelekeo wa Kingono, wagonjwa wanaotumia bangi kwa ajili ya matibabu na hali ya kuwa mtu aliyenusurika katika mzozo wa kinyumban.
    - **Makazi:** Ukoo, Hali ya Uraia, Rangi, Ulemavu, Hali ya kuwa na Familia, Utambulisho wa Kijinsia, Ubainishaji wa Jinsia, Vitambaa vya Nywele na Kichwani, Asili ya Utaifa, Mahalipa Kuzaliwa, Lugha Inayopendelewa, Mbari, Dini, Jinsi, Mwelekeo wa Kingono, Hali ya kuwa Mhadhiriwa wa Mizozo ya Kinyumbani.
    - **Malazi ya Umma:** Ukoo, Hali ya Uraia, Rangi, Ulemavu, Hali ya kuwa na Familia,Utambulisho wa Kijinsia,Ubainishaji wa Jinsia,Vitambaa vya Nywele na Kichwani, Asiliya Kitaifa, Mahalipa Kuzaliwa, Lugha Inayopendelewa, Mbari, Dini, Jinsi, Mwelekeo wa Kingono.

## *Nani Anaweza Kuwasilisha Malalamiko?*

- Mtu yeyote anayehisi amebaguliwa katika jiji la Pittsburgh anaweza kuwasilisha malalamiko. Makundi ya watu au mashirika yanaweza kuwasilisha ikiwa wanahisi wamebaguliwa au wanamtetea mtu ambaye amebaguliwa.
- Kuwasilisha malalamiko, tembelea tovuti yetu kwenye www.pittsburghpa.gov/chr au tupigie simu kupitia (412) 255-2600 ili kuweka miadi ya kusikilizwa.

Kwa maelezo zaidi, tupigie simu au tembelea tovuti yetu **www.pittsburghpa.gov/chr**